MWONGOZO WA MWALIMU

# MASUALA YA USHIRIKA

CHURCH OF GOD OF PROPHECY

# YALIYOMO


- **SOMO 1 ============ 2**
  Maisha Mapya ndani ya Kristo
- **SOMO 2 ============ 7**
  Kwa Nini Uwe Mshirika?
- **SOMO 3 ============ 11**
  Kanisa Letu la Mahali Pamoja
- **SOMO 4 ============ 15**
  Ni Kubwa Kuliko Sisi
- **SOMO 5 ============ 25**
  Nini Kinachofuata?
- **REJEA ============= 31**
- **VIAMBATANISHI MUHIMU 32**



# DIBAJI

**Walioshiriki:** Shukrani zetu za dhati kwa waliohusika katika kufanikisha somo hili: Waandishi walioshiriki ni kama wafuatao: Bishop Timothy Coalter na Brian Sutton. Machangizo mengine yalifanywa na Kanisa la Church of God of Prophecy la (Cleveland, TN) na Uongozi wa Idara ya Maendeleo na Uanafunzi wa Kanisa la Church of God of Prophecy.

Shukrani za dhati kwa Idara ya Maendeleo na Uanafunzi kwa kuongoza na kumaliza kazi hii, wakishirikiana na Masomo ya Jumapili/Huduma ya Elimu ya Kikristo.

**Imekamilishwa na:** Kathryn H. Creasy, Darren Schalk

**Wahariri::** Becky Chaffin, Kathryn H. Creasy, Marsha Robinson, Darren Schalk

**Advisors:** Bishops Gary Adkins, J. Milton Atkins, Daryl Clark, M. Scott Lee, Trevor Reid, Jack Sheets, Duke Stone, and Pastor Jonathan Olavarria

**Mpangilio:** Jonathan Lovvorn, Tony Orona

**Ruksa ya Kunakri:**

Hakimliki 2020 imetolewa na Ofisi za Kimataifa za Church of God of Prophecy.

Ruksa ya kutoa nakala kwa ajili ya matumizi ya kanisa ya mahali pamoja. Copyright © church of God of Prophecy International Offices. Membership Matters by Church of God of Prophecy International offices, P.O BOX 2910, Cleveland, TN 37320-2910. www.cogop.org.

Zingatia, vifungu vya maandiko vimechukuliwa kutoka kwenye toleo la King James la Biblia Takatifu.

Nukuu ya maandiko vilivyo andikwa NIV vimechukuliwa kutoka katika Biblia Takatifu, New

International Version ® NIV® Copyright © 1973, 1978,1984,2011 na International Bible Society. Imetumika kwa ruhusa ya Zondervan Publishing House. Haki zote zimeifadhiwa.

Maandiko yaliyowekea alama TNIV yamechukuliwa kutoka Biblia Takatifu (Today's New

International Version TM TNIV) ® Copyright © 2001, 2005 ya chama cha biblia cha Amerika. Imetumika kwa ruhusa

# SOMO 1
# MAISHA MAPYA NDANI KRISTO

## UTANGULIZI:

Karibu katika darasa la ushirika kwa ajili ya kanisa la ( jina la kanisa liandikwe hapa). Ndani ya wiki chache zijazo, tutawatambulisha kwa kanisa, na labda kwa waamini wengine wanaokuja kanisani na hata wewe mwenyewe tunavyoendelea kujifunza kuhusu sisi ni nani ndani ya Kristo.

## TUKIO LA KUFUNGUA

*Jaza karatasi iliyoandikwa Kuhusu Mimi, inayopatikana katika rejea za ziada kwenye ukurasa wa mwisho. Muombe kila mwanafunzi ajitambulishe mbele ya darasa kwa kujibu maswali yafuatayo:*

- Jina lako nani
- Ulizaliwa wapi
- Je!ni sehemu gani ya siku unayoipenda?
- Ni chakula kipi upendacho? Kwa nini?

*Mara baada ya kumaliza, kukusanya karatasi Kuhusu Mimi kwa kumbukumbu za kanisa.*

## YALIYOMO KATIKA SOMO

# 1 MAISHA YAKO NDANI YA KRISTO

**NINI KINATAKIWA KWA AJILI YA USHIRIKA WA KANISA?**
Matendo ya Mitume 2:47 inasema “Kila siku Bwana akaliongeza kanisa kwa wale watu waliokuwa wakiokolewa.” Wokovu binafsI—na kukiri dhambi zako na kuanza kumwamini Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wako—hiki ndicho kinachotuunganisha sisi kama Wakristo na ndio kigezo cha kwanza kabisa cha ushirika kanisani.

**NAWEZAJE KUFAHAMU KUWA MIMI NI MKRISTO.**
Yohana aliandika barua yake ya kwanza ili kuwawezesha wakristo wawe na uhakika wa wokovu walioupata. Nimewaandikia ninyi mambo hayoili mjue ya kuwa mna uzima wa milele ninyi mnaoliamini jina la Mwana wa Mungu. (1 Yohana 5:13). Barua hii ya Yohana inatupa vigezo sita ambavyo vinatupa uhakika wa kuwa sisi ni Wakristo.

## BWANA AKALIZIDISHA KANISA KILA SIKU KWA WALE WALIOKUWA WAKIOKOLEWA MATENDO YA MITUME 2:47

Tafadhali soma vifungu vifuatavyo na ukamilishe kila sentensi hapo chini.

**1 Yohana 1:7**
Ninajua mimi ni Mkristo ikiwa **ninatembe kwenye nuru.**

**1 Yohana 1:9**
Ninajua mimi ni Mkristo ikiwa **ninatubu dhambi zangu**

**1 Yohana 2:3**
Ninajua mimi ni Mkristo ikiwa **ninatii amri Zake**

**1 Yohana 3:9**
Ninajua mimi ni Mkristo ikiwa **siishi Maisha ya dhambi**

**1 Yohana 3:14**
Ninajua mimi ni Mkristo ikiwa **ninawapenda watu wote katika Kristo.**

**1 Yohana 5:10**
Ninajua mimi ni Mkristo ikiwa **ninaamini katika Mwana wa Mungu.**

**NIFANYE NINI BAADA YA KUOKOKA.**
Unapokuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo, maisha yako yanabadilika katika njia mbalimbali. Mistari ya Biblia ifuatayo inaonesha aina tatu za "Matunda" (anachokifanya Kristo ndani yako ambacho wengine watakiona) kama matokeo ya Wokovu.

Tafadhali soma mistari hii ya Biblia na kisha jibu maswali yanayofuata.

**Mathayo 28:19; 1Petro 3:21**
Waamini wafanye nini kinachodhihirisha kwa nje kuwa wameokoka?
**Wabatizwe kwa Maji Mengi**

Mtu anawezaje kujitambulisha kwa Kirsto katika hili tukio la wazi?
**Kufuata mfano wa Yesu na mafundisho Yake katika kanisa.**

**Mathayo 26:26-29; 1 Wakorintho 11:23-26**
Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini katika kila mistari hii?
Mathayo 26: 26-29 **Chukua, Kula, Kunywa**
1Wakoritho 11:23 -26: **fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu . tangazeni kifo cha Bwana mpaka atakaporudi.**



Aina ipi ya Ibada maalumu ambayo waamini wa nyakati za leo wameelezwa waishiriki pamoja? **Kula mkate, uliowakilisha mwili Wake uliovunjika, na kunywa divai kwenye kikombe ambacho kiliwakilisha damu yake iliyomwagika kwa ajili yao katika Komunio au Meza ya Bwana.**

Ni kwa namna gani kushiriki ibada kunaashiria ushirika pamoja na Kristo. **Tunaposhiriki, tunakumbuka kujitoa kwake na kungojea kurudi kwake.**

**MAISHA YANGU YATAKUWAJE BAADA YA WOKOVU?**
Kukiri imani yako ndani ya Kristo na kumpokea Yeye kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako kunaleta upya katika mitazamo na mawazo maishani mwako. Wagalatia 5:22, 23 inatupa kwa kiasi tabia za Roho Mtakatifu ambazo atazifanya ndani ya mwamini.

**SOMA Wagalatia 5:22.23**
Taja tabia tisa za matunda ya Roho. Tambua kuwa tabia zote hizi hazijitokezi ndani ya muamini kwa wakati mmoja, bali ni tabia ambazo zinajitokeza moja baada ya nyingine kadri muamini anavyozidi kukua katika Kristo.

**1. Upendo**
**2. Furaha**
**3. Amani**
**4. Uvumilivu**
**5. Fadhil**
**6. Wema**
**7. Imani**
**8. Upole**
**9. Kiasi**

Ni tabia zipi hapo juu zinajidhihirisha katika maisha yako?

______________________________________________

Tabia zipi ambazo unaziona zinakuwai ndani yako?

______________________________________________

*Wambiie wanafunzi walio tayari wawasilishe majibu yao*

# 2 USHUHUDA WAKO NDANI YA KRISTO

**UNAO USHUHUDA WA KUSIMULIA!**
Ili kuvutia wateja kwenye biashara yako, matangazo mara zote yanatakiwa yaonyeshe kile

## *KILA SIKU JIANDAE KUTOA JIBU KWA KILA MMOJA ANAYEJUHULIZA*

1 PETER 3:15 NIV

kinachovutia kwenye hiyo bidhaa yako. Kwa kuwa sasa wewe uko na Yesu, WEWE ni USHUHUDA ULIO HAI kuwa uwezo wa Yesu wa kubadili maisha ya watu upo na unaonekana. Unao ushuhuda wa tofauti, ambao ni ushuhuda katika Kristo na ni wewe tu unaweza kuusema.

Japokuwa si mara nyingi hasa nyakati za leo kwa Makanisa kuwa na "Ibada za shuhuda", ambapo mtu mmoja baada ya mwingine wanasimama mbele na kushuhudia , kile ambacho Mungu amefanya na anachoendelea kufanya katika maisha yao. Shuhuda zao za uaminifu wa Mungu na kujibiwa Maombi yao kunawatia moyo wengine waendelee kumwamini Mungu pia.

Biblia imeandikwa kama ushuhuda. Ni ushuhuda wa Mungu kwa mwanadamu. Ni habari juu ya upendo mkuu wa Mungu kwetu sisi. Ni HABARI ya KWELI! Ni habari ya Mungu kumtuma Mwanae(omitted a repeated line )ili awakomboe wanadamu kutoka katika dhambi zao. Kama unamjua Mungu, UNAO USHUHUDA WA KUSEMA. Mungu amekupa ushuhuda na ushuhuda wako ni wa MUHIMU sana kuweza kuwafikia wengine walioko karibu nawe.

Sisi kama "Wapentekoste" je tuna utayari wa kushiriki katika kutoa ushuhuda wa Mungu? Je tuna utayari wa kushuhudia kile ambacho Mungu amefanya katika maisha yetu? Marafiki na ndugu zetu wasioamani hawatapenda kusikia shuhuda za watu wengine kuhusu kile ambacho Mungu aliwafanyia. Wanapenda kusikia ushuhuda wako wa kile ambacho Mungu amekufanyia. Wanataka kufahamu kama Mungu anaweza kufanya na kwao pia.

**JIANDAE KUSHUHUDIA**

"……. Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu;" (1 Petro 3:15) Zoezi linalofuata litakuandaa uweze kushuhudia.

**WEWE NI NANI—KK NA BK**

Msalaba wa Kristo ndio kitu kinachoigawa historia ya wanadamu. Matukio yamegawanywa katika KK (Kabla ya Kristo) au BK (Baada ya Kristo). Ushuhuda wa muamini pia unatakiwa uwe na pande mbili:

**KK – Maisha yao kabla ya kuanza uhusiano na Yesu**
**BK – Maisha baada ya Yesu kuingia ndani.**

Yafuatayo ni mazoezi yatakayokuwezesha kuweza kutoa ushuhuda wako kila pale Mungu anapokupa nafasi ya kufanya hivo.



**Hatua 1: Mimi nilikuwaje KK (maisha yangu ya kale)**
Andika haya moja au mbili kuelezea maisha yako kabla hujaokoka.

**Hatua 2: Kugeuzwa**
Elezea kile kilichotokea baada ya kuanza uhusiano na Yesu. Kitu gani kilikufanya utambue kuwa Yeye ni jibu? kitu gani hasa ulikifanya?

**Hatua 3: Mimi ni nani BK (maisha yangu mapya)**
Elezea jinsi ulivyo wa tofauti kwa Yesu anaishi ndani yako. Elezea jinsi gani Misimamo, tabia na jinsi unavyohusiana na watu kulivyobadilishwa? Eleza jinsi unavyobadilika na kukua kwa sababu Kristo yuko ndani yako.

Baada ya kuandika hizo sehemu tatu za maisha yako, mshirikishe mtu katika darasa lako. Baada ya hapo tafuta fursa za kutoa ushuhuda binafsi wa “Maisha Ndani ya Yesu” kwa mtu mwingine ambaye anahitaji upendo na msamaha wake.

# SOMO 2
# KWA NINI UWE MSHIRIKA?

## UTANGULIZI

Kipindi hiki kitajadili kwa nini Wakristo tunahitaji tuwe na Kanisa la Mahali Pamoja. Kuwa mshirika ni fumbo, lakini ni zaidi ya hapo. Tumaini letu hasa ni kuwa na waamini wa Yesu Kristo walioungana katika umoja, katika mwili wa Kristo – katika ushirika wa waaminio na katika maisha ndani ya Kristo.

## TUKIO LA UFUNGUZI

*Katika somo la mwisho, tulijaza karatasi za KUHUSU MIMI. Angalia ikiwa mtu yeyote darasani anaweza kukumbuka habari aliyojifunza kwa wanafunzi wengine. Tumia hii kama kichocheo cha wanafunzi kutambulisha darasani, na labda pokea washiriki wowote wapya. Ikiwa wanafunzi wapya wapo, waagize wajaze karatasi ya KUHUSU MIMI kutoka kwenye somo lililopita (inayopatikana katika rejea za ziada)*

*Uliza swali hili:*
"Kwa nini mtu anahitaji kuhudhuria kanisani?"

*Leo, tutajadili baadhi ya dhana za msingi kuhusu Kanisa na kwa nini ni muhimu mtu aji-unge rasmi na Kanisa.*

## YALIYOMO KATIKA SOMO

# 1 MKRISTO ANAHITAJI KANISA KWA SABABU....

Muumba wetu alituumbwa ili tuweze kuishi tukihusiana na watu wengine. Katika hekima za juu sana, Yesu alitupa namna ya sisi kama waamini wake kuungana pamoja.

"Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake." (Warumi 12:5)

Kuna faida nyingi za kuwa kiungo katika Mwili wa Kristo. Tafadhali soma maaandiko yafuatayo na kisha umalizie maneno yanayotakiwa.

> ***BALI MUNGU AMEVITIA VIUNGO KILA KIMOJA KATIKA MWILI KAMA ALIVYOTAKA. LAKINI KAMA VYOTE VINGEKUWA KIUNGO KIMOJA, MWILI UNGEKUWA WAPI? LAKINI SASA VIUNGO NI VINGI, ILA MWILI NI MMOJA.***
> ***(1WAKORINTHO 12:18-20).***

- Warumi 12:5; Waefeso 2:19
Kanisa linatuunganisha sisi pamoja na waamini wengine katika **Ushirika wa Kikristo**.

- Wagalatia 6:1-2; Waebrania 10:24-25
Kanisa linatoa familia ya Kiroho **ili kukusaidia kubeba changamoto** na kwa **kukutia moyo** kwako na kwa maisha yako katika Kristo.

- 1Wakorintho 12:4-17
Kanisa linakupa semehu ya kutambua na kutumia **Karama zako za Kiroho**

- Matendo 20:28; Waebrania 13:17
Kanisa linakuweka chini ya **Msaada** wa kiroho wa viongozi wamcha Mungu.

- Waefeso 4:11-13
Viongozi wa kiroho kanisani **wanakuandaa** kwa ajili ya kazi na huduma na kukusaidia **kukua** katika Kristo.

# 2 HEBU JARIBU KUFANANISHA

**MKRISTO BILA KANISA NI SAWA NA ...**

- Na mwanajeshi bila **kikosi**
- Mwanamziki bila **kikundi**
- Kondoo bila **kundi**



# 3 KIPI UKITARAJIE KUTOKA KWENYE KANISA LAKO...

**Mahali penye upendo**
Kwa kutambua hitaji letu la muhimu la kuthaminiwa, tunatakiwa kutengeneza mazingira yatayowafanya watu wajisikie kukaribishwa, kuheshimiwa, na kupendwa. Mahusiano ya muda mrefu yanajengwa katika misingi ya malengo na makusudi yanayoendana. Kazi mbalimbali Kanisani zinasaidia Wakristo kukua na kushiriki pamoja.

**Kujitoa kwa ajili ya mafundisho ya msingi katika Imani.**
Tunatakiwa kujitoa kwa ajili ya mafundisho ya msingi yaliyojenga imani ya Kikristo. Hii inahusisha imani yetu katika Yesu kama Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na bikira, aliishi bila kutenda dhambi, alikufa msalabani kwa ajili ya kulipa mshahara wa dhambi zetu, alifufuka na kushinda dhambi na mauti, na atarudi tena. Yesu Kristo ndiye msingi wa imani na ibada yetu.

**Mahali palipo na Roho Mtakatifu**
Tunaamini kuwa kuhubiri Injili chanya ya Neema inawapa nguvu Wakristo kuishi katika misingi ya neno la Mungu. Kwa hiyo tunachochea uwepo wa Roho katika kusifu, kuabudu na mafundisho sahihi ya Kibiblia na Mahubiri tukiwa na ufahamu kuwa Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yetu.

**Huduma kwa familia**
Tumekusudia kuhamasisha na kuimarisha umoja wa kifamilia. Jukumu hili linaonekana kwa huduma ya kichungaji kwa watoto na vijana, tukigusa maisha yao katika wakati muhimu kabisa wa ukuaji wao, lakini pia kuhudumia watu wote wa rika zote.

**Msaada wa Kichungaji**
Pale matukio magumu yanapotupata, kama magonjwa na kupoteza ndugu na jamaa. Wachungaji wapo pamoja na wewe katika mapito hayo wakikutia moyo na kukupa msaada wa Kiroho.

**Roho ya Ukarimu**
Tunatoa kwa ukarimu katika jumuiya, nchini na hata ulimwenguni kote. Kanisa letu haliko kuhudumiana sisi kwa sisi tuu. Kanisa letu linatoa kwa ukarimu katika utume wa aina tatu.

**Mahali Pamoja::** Kupitia huduma ya Mahali Pamoja Kanisani..

**Katika nchi:** Sawa na maelekezo ya Mungu, tutatoa kwa washirika wengine ndani ya

nchi yetu, lakini pia kuwezesha huduma kama makambi ya vijana na watoto katika nchi yetu.

**Ulimwenguni:** Kupitia huduma kwa Ulimwengu wote, wakala wa umisheni wa kanisa la Church of God of Prophecy, Kanisa letu linaunganishwa kusaidia huduma maalumu. Makusanyo yanapelekwa kwa Harvest Partiner kupitia Huduma kwa Ulimwengu (Global Mission). Hapo zawadi hubadilishwa na kuwekwa katika thamani ya pesa na kutumwa kwa viongozi wa kitaifa. Waangalizi wa Mabara na Ofisi za Kimataifa wanashirikiana kuhakikisha mfumo wa uwazi uko vizuri katika maeneo yote duniani.

### Fursa za kutumika

Ili kukua katika uhusiano wako na Kristo, unahitajika ujihusishe kikamilifu katika moja ya huduma ya huduma hizi. Kanisa letu la mahali linajitoa kukusaidia kufikia mojawapo ya huduma zilizopo au kwa kukushirikisha kwenye huduma mpya mahali ambapo Mungu atakuwa anakuongoza.

## HITIMISHO

Malizia somo hili kwa kusoma Warumi 12:3-21.

fikiria juu ya majukumu yote ya kanisa yaliyoko katika kifungu hiki, na pia majukumu ya kila mmoja na uwepo wetu na kujitoa kwetu katika kanisa kunavyoweza kusaidia kufanikisha haya majukumu.

# SOMO 3

# KANISA LETU LA MAHALI PAMOJA.

## INSTRUCTOR'S NOTE

*This lesson is intended to give you a way to present the information pertinent to your local church. We will offer you an outline to do so. Each section will call for information from you. The information needed will hopefully be readily available, but if not, we know the search for the information needed to present your church currently and historically will be well worth the time given.*

## UTANGULIZI

Wiki hii yote tuajifunza kuhusu Kanisa LETU! Japokuwa sisi ni sehemu ya kanisa kubwa la Waamini wa Ulimwengu, tumechagua kuwa washirika wa (Jina la kanisa lako hapa). Kwa hiyo tujifunze vitu vichache kuhusu Kanisa letu!

## YALIYOMO KATIKA SOMO:

## 1 KANISA LETU KIHISTORIA

Kanisa letu lilianzishwa mwaka wa______________________________ na Mchungaij (jina la Mchungaji) ________________________________.

Kanisa letu mwanzo kabisa lilikuwa eneo la ________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________.

**ORODHA YA WACHUNGAJI WALIOWHI KUHUDUMU KANISANI**

**MIAKA WALIYOHUDUMU**

**TAARIFA NYINGINE MUHIMU ZA KIHISTORIA KUHUSU KANISA LETU**

# 2 KANISA LETU LEO

**MAADILI YETU YA MSINGI (OUR CORE VALUES) -- Kama yapo**


**TAMKO LA LENGO (OUR MISSION STATEMENT) -- kama lipo**

**TAMKO LA MAONO (OUR VISION STATEMENT) -- kama lipo**

**HUDUMA TULIZONAZO HADI SASA.**

*Kwa wakati huu, waalike viongozi wa huduma katika kanisa lako kutoa mada fupi kuhusu maeneo yao ya huduma. Wahimize kutoa taaarifa juu ya jinsi gani washirika wapya wanaweza kujihusisha kutumikia katika kila eneo la huduma.*

**Sehemu za huduma zinajumuisha:**
Huduma ya Vijana
Huduma ya watoto (chekechea, shule ya awali, na msingi)
Huduma ya Wanaume / Wanawake
Huduma ya Sauti / Video
Huduma ya ufikiaji (huduma ya chakula, fadhili, makazi ya muda, nk.)
Huduma ya Misheni
Shule ya Jumapili / Elimu
Huduma ya Mchungaji
Huduma ya Vikundi Vidogo
Huduma ya Maombezi
Huduma ya Ukarimu
Miradi na Huduma mbali mbali (huduma gerezani, mkakati ng'arisha viatu, nk)
Huduma za kusaidia (kukaribisha, maegesho wahudumu, nk.)



# 3 KANISA LETU KESHO

*Hii ni fursa ya mchungaji kushirikisha maono yake yajayo ya Kanisa kwa waamini.*

*Alika washirika waelezeeni kwa namna gani Kanisa linaweza kuwasaidia na kuwapa uwezo wa kufanya kazi ya Mungu ambayo wanatakiwa kufanya.*

# 4 UKIRI WA MSHIRIKA

Mkristo anajiunga kanisani kwa kukiri maneno ya ahadi kama washirika wengine wote walivyofanya. Lengo la ahadi (agano) hiyo ni kutangaza wazi wazi utayari wako kutii mafundisho ya Kristo na kujitoa kwako binafsi kwa Neno lote la Mungu.

Katika ibada, Mchungaji ataalika watu wanaopenda kujiunga na kanisa kwa kusema ahadi ya kujiunga pamoja na kanisa wapite mbele. Atakuomba ushike Biblia mkononi kwako atakuambia useme "Nitatii" kila atakapokuwa anauliza maswali yafuatayo.

**"Je unaahadi kwa dhati mbele ya Mungu na mashahidi hawa kuwa:**

- **Unaikubali Biblia kuwa ni Neno la Mungu.**
- **Kuamini kutenda sawasawa na mafundisho yake yanayogawanyika sawa na Agano Jipya likiwa mwongozo wa Imani, Utendaji na utawala na nidhamu na**
- **Kutembea katika nuru kadri ya ufahamu na uwezo wako?"**

Watu ambao walikwisha toa tamko kama hili kwenye kanisa lingine la Church of God of Prophecy wanatakiwa kuomba uongozi ili ushirika wao uhamishwe. Utoaji na upokeaji wa hamisho hizo unafanywa katika vikao vya kawaida vya kanisa. Ni agano ambalo linatuunganisha katika kanisa ulimwenguni kote, kwa hiyo ni muhimu kuwa kila muamini aseme ahadi hiyo. Kwa hiyo katika kanisa la Church of God of Prophecy, kama ilivyo kwa madhehebu mengine, uhamisho unafanywa kutoka kanisa moja kwenda lingine ndani ya dhehebu. .

Ushirika unaamishwa au kusisitishwa kupitia barua iliyoandikwa na mshiriki na kupitishwa na baraza la kanisa la mahali pamoja. Ushirika unaweza kusitishwa kama sehemu ya kupewa nidhamu kutokana na vitendo vya dhambi au maisha yasiyo ya Kimungu.

# SOMO 4
# NI KUBWA KULIKO SISI.

**Utambulisho wetu kama sehemu ya Church of God of Prophecy.**

## 1 Church of God of Prophecy ni nani?

Kanisa hili ni sehemu ya muunganiko mkubwa kiulimwengu ujulikanao kama Church of God of Prophecy. Tumeungana na washirika na Makanisa mengine Ulimwenguni mwote ambao pia wanathamini Maombi, Mavuno, Kuendeza Viongozi, Uwakili na Huduma. Umoja huu unatengeneza nguvu kubwa sana ya muunganiko ambayo inatusaidia sisi kutimiza wito wa Mungu.

Church of God of Prophecy ni kanisa lililo na hamasa kubwa, likiwa na waamini ulimwenguni kote, walioungana katika kuabudu, wakishirikiana bega kwa bega kueneza upendo wa Mungu na injili ya tumaini kwa mioyo iliovunjika.

Kila baada ya saa 24 ulimwenguni kote:

- Zaidi ya watu 500 wanapokea Wokovu
- Zaidi ya watu 200 wanabatizwa Ubatizo wa maji mengi
- Zaidi ya maeneo 10,000 ya kuhubiri injili yanakuwa yanatumika

Angalau Kanisa moja linakuwa wazi kwa ajili ya kuifikia jamii inayozunguka kanisa laa Mahali Pamoja kupitia juhudi za vuguvugu hili.

Church of God of Prophecy lina zaidi ya Washirika milioni moja, wanaoabudu katika Makanisa 10,000 na misheni katika nchi zaidi ya 130 duniani. Karibu asilimia 90 ya waamini wote ulimwenguni wanatoka nje ya bara la Amerika ya Kaskazini.

Katika theolojia ya kawaida, Church of God of Prophecy ni vuguvugu la Kiprotestanti, Kiinjilisti, utakatifu wa Wesleya, la Kipentekoste ambalo linaamini katika uhuru halisi wa mtu uko katika Wokovu.

# 2 KUHUSU SISI

**Maono yetu**
Kuupatanisha Ulimwengu kwa Kristo kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu.

**Malengo yetu**
Church of God of Prophecy ni Kanisa linamtangaza Yesu, Utakatifu, ujazo wa Roho, kuwafanya Mataifa Wanafunzi wa Yesu, upandaji wa Makanisa na shahuku ya umoja wa Kikristo.

**Vipaumbele vyetu**
Vipaumbele vyetu ni falsafa au kanuni ya utendaji kazi zinazoongoza kazi zinazofanyika ndani ya taasisi pamoja na mahusiano yake na jamii inayozunguka. Uongozi wa Church of God of Prophecy umetanabaisha vipaumbele vitano vya Kanisa. Navyo ni Maombi, Mavuno, kuendeleza Viongozi, Uwakili, na Huduma.

**Tamko letu la Imani**
Tunaamini katika Utatu Mtakatifu – Mungu mmoja, aliye katika Nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

Tunaamini katika Mungu mmoja, Baba, Muumba wa mbingu na dunia, na vitu vinavyoonekana na visivyo onekana.

Tunaamini katika Mungu mmoja, Baba, muumba wa Mbingu na Nchi na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Tunaamini katika Bwana, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa kwa Baba. Vitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake. Ni Mungu halisi na Mwanadamu halisi. Alitungwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na alizaliwa na Bikira Maria. Aliteswa, alikufa, akazikwa, na siku ya tatu akafufuka kutoka (katika-omit highlighted word) wafu. Akapaa na kukaa mkono wa kulia wa Baba, atarudi ili kuwahukumu walio hai na walio kufa. Ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Tunaamini katika Roho Mtakatifu, Bwana na Mpaji wa maisha, Yeye atokaye kwa Baba. Yeye ni Mwalimu, Mfariji, Msaidizi, na Mpaji wa Karama za Rohoni. Kupitia Yeye, kazi ya Yesu ya kuokoa na kutakasa inafanyika ndani ya Maisha ya mwamini. Ndiye anayeleta uwepo wa Mungu katika maisha ya Mkristo na kwa Kanisa. Baba amemtuma Mwanae abatize kwa Roho Mtakatifu. Kunena kwa lugha na kuzaa matunda ya Roho ni ishara za ujazo wa Roho Mtakatifu katika Agano Jipya.

Tunaamini kuwa Wokovu unapatikana kwa neema kupitia Imani kwa kifo cha Yesu Msalabani; na kwamba Alikufa badala yetu. Dhambi za waamini zinasamehewa kupitia damu yake iliyomwagika Msalabani. Tunaamini kuwa uponyaji wa nafsi, mwili, roho unapatikana kwa muamini kupitia damu ya Yesu Kristo na nguvu ya Roho Mtakatifu.

Tunaamini kwamba neema ya Mungu huleta msamaha na upatanisho kwa wale ambao wanatubu, na vile vile kuwabadilisha katika utakatifu, kuwawezesha kuishi maisha kama ya Kristo. Utakaso ni kazi dhahiri ya neema na mchakato wa maisha yote wa mabadiliko katika muamini aliyeletwa na damu ya Yesu, Neno la Mungu, na nguvu ya uweza ya Roho Mtakatifu.

Tunaamini katika Kanisa moja takatifu, la ulimwengu wote, linaloundwa na waamini wote wa kwelikatika Yesu Kristo, kutoa Ushirika na Wito wa huduma kwa wanaume na wanawake wa jamii zote, Mataifa, tamaduni,na lugha. Tunaamini umoja wa kiroho na kufikia umoja wa Kanisa unadhihirika.

Tunaamini kwamba Biblia — Agano la Kale na Jipya — ni Neno la Mungu lililohuishwa. Biblia ni Ufunuo wa Mungu mwenyewe na mapenzi Yake kwa wanadamu, inayojitosheleza kwa mafundisho katika wokovu na maishaya Kikristo ya kila siku. Agano Jipya ni kanuni ya imani na matendo ya Mkristo.

Tunaamini kwamba mwishowe Mungu atapatanisha vitu vyote Mbinguni na Duniani katika Kristo. Kwahivyo,tunatazamia Mbingu mpya na Dunia mpya ambayo haki hukaa.

# 3 KANISA LA LEO

Leo, muundo wa taasisi ya Church of God of Prophecy lipo na linafanya kazi katika viwango vitatu vinavyotegemeana:

- Kimataifa
- Jimbo, Mkoa, au Kitaifa
- Mahali Pamoja

**Kimataifa**

Ngazi za kimataifa hufanya kazi kutoa mtandao mkubwa wa msaada na mwingiliano kwa huduma za Kanisa katika Mataifa mengi Ulimwenguni. Inaongozwa na kikundi chenye Vipawa ya Viongozi wenyeuzoefu wanaotajwa kama wakuu wa jumla. Wanachaguliwa kutoka kwa Uongozi wa Kanisa kote ulimwenguni, wakuu wa jumla hutoa uangalizi wa Kiroho, Maono, na mwelekeo kwa Kanisa kwaujumla. Wanaongozwa na Mwangalizi Mkuu, Askofu aliyechaguliwa kutumika kama mwangalizi wa Mikutano ya Kimataifa ya Kanisa. Anawajibika kwa kuandaa majukumu mapana ya kazi za Uongozi wenye tija na majukumu ya kiutawala.

Ofisi za Kimataifa za Kanisa, zilizoko Cleveland, Tennessee, Marekani zimeundwa kutoa huduma muhimu za msaada na shughuli za kipekee za huduma kwa Ulimwengu kupitia msaada wa kifedha, Uongozi hamasishi, na kukuza maadili ya msingi kote Ulimwenguni.

Kila baada ya miaka miwili, Uongozi na Walei kutoka Ulimwenguni kote huja pamoja kuunda Barazala Kimataifa – chombo kinachofanya maamuzi juu ya mafundisho ya Kanisa. Mikutano ya Kimataifa inashughulikia mafunuo ya Kibiblia yanayoendelea, pamoja na matakwa ya kiutengaji Kimataifa, nahutoa mwendelezo kwa harakati hiyo kupokea mwongozo kwa umoja kama familia ya Kanisa. Kwa wikhii nzima ya ukaribisho duniani kote, iko wazi kwa wote, kunampa kila Mshirika wa Kanisa fursa yakushiriki katika kuendeleza shughuli, na pia kuhudumiwa na huduma tofauti, huduma zilizojaa Roho kutoka Ulimwenguni kote.

Sio tu kweli za Kibiblia kama vile Toba, Kuzaliwa Upya, Utakaso, na Utakatifu wa maisha uhubiriwa wakati wa Mkutano, lakini pia watu huishi hayo mafundisho katika Makanisa Ulimwenguni kote. Watuwengi wamegundua kwamba ili kulielewa Kanisa, ni mhumu ushiriki mkutano wa Kimataifa.

Church of God of Prophecy liliinuliwa na Mungu kuwa udhihirisho wenye nguvu kwa Ukristo wa Agano Jipya. Agano la maneno linaloonekana wazi na hadharani linawaunganisha Waumini kwenye Church of God of Prophecy, kwa Kanisa la Mahali Pamoja na la Kimataifa pia. Agano hili halileti Wokovu, lakini linafanya jukumu linalohitajika katika ukuaji wa kibinafsi na ukomavu wa Kiroho kwa kumweka Muumini katika jamii na wengine.

**Jimbo, Mkoa, au Kitaifa**

Katika kiwango cha Jimbo, Mkoa, au Kitaifa hutoa Uongozi na msaada ndani ya eneo lililotambuliwaa ili kukamilisha kazi ya Kanisa kwa njia bora. Waangalizi huteuliwa na Mkuu wa eneo lao kuongoza maeneo haya kama Viongozi Watumishi. Wajibu wao ni pamoja na kuhudumia, kusimamia, na kuteua Wachungaji waliohitimu katika maeneo yao maalum, na pia kuhamasisha Mkoa wao katika upelekajiwa Injili.

**Kanisa la Mahali Pamoja**

Makanisa ya Mahali Pamoja ni moyo wa Church of God of Prophecy, hutoa mahitaji ya haraka ya makutano maelfu kwa maelfu katika majiji, miji, na jamii ambayo utume wa Kanisa unafanywa kilasiku. Ni katika kiwango hiki watu huja kwa Kristo, hubatizwa, na huletwa katika ushirika, na kufundishwa kuishi maisha ya Kikristo ya ushindi.

Makanisa ya Mahali Pamoja yanaongozwa na Mchungaji mwenye sifa, mwenye Leseni, wanaoteuliwana Mwangalizi husika ambaye anafanya kazi kwa kushirikiana na Makanisa ya Mahali hapo. Mchungaji hutumika kama Kiongozi wa Kiroho na kiutawala, akitafuta mwongozo wa Mungu kwa ajili ya Waumini wake.



Ibada ya kushiriki, kuhubiri kwa nguvu, ufikiaji wa kiinjili wa vitendo, shughuli ambazo husaidia familia ya leo, Mafundisho ya Kibiblia, ukuaji wa kibinafsi kupitia ushiriki wa huduma, na mazingira ya kukubali mazingira ya kifamilia ambayo yanawasilisha upendo wa Mungu yote yamejumuishwa ndani ya maisha ya Church of God of Prophecy.

Madhehebu mengine yamekaribishwa katika Church of God of Prophecy katika nyakati za hivi karibuni. Wameliona ni Kanisa lenye usafi wa kibiblia, lenye muundo mzuri wa taasisi, mtandao wa uwajibikaji ulio shirikishi, na kanisa lililojitoa kuhudumia watu katika hali ya kisasa ya leo.

# 4 KIHISTORIA YA CHURCH OF GOD OF PROPHECY

Harakati ya Church of God of Prophecy ilianza zaidi ya miaka mia moja iliyopita katika Mioyo ya Waumini wenye bidii katika milima ya vijiji vya Kaunti ya Cherokee, Carolina.ya Kaskazini

**UMOJA WA KIKRISTO**

Kuanzia mwanzo wake, harakati ya Church of God of Prophecy ilikuwa na wanaume na wanawake ambao walijulikana na kiu yao kubwa kwa Mungu. Kiu hii iliwasukuma zaidi kutoka uhusiano wa Kikristo wa kawaida hadi Umoja wa Waamini, waliojitoa kwa mafundisho ya Biblia nzima. Kikundi chawatu kilikusanyika katika nyumba ya kukutania ya Barney Creek huko kaunti ya Monroe, Tennessee, mnamo Agosti 19, 1886. Walikutana pamoja na himizo la Richard Spurling, Sr. na mtoto wake, R.G. Spurling. James Stone anasema, “Kwa Ulimwengu, kusanyiko hili dogo lilikuwa na umuhimu mdogo. Kwao, ilikuwa juhudi ya kujaribu kupata mapenzi ya Mungu na kujitenga na imani na mila za jadi. ”[1]

R. G. Spurling aliwahubiria wale waliokuwepo Barney Creek, akiwataka kukata uhusiano na imani zajadi na kujiunga na Kanisa la Agano Jipya. Watu wanane walijitokeza siku hiyo na kujiunga pamoja nakuunda Mkutano ambao ulijulikana kama Umoja wa Kikristo.

Kulikuwa na sababu kadhaa zilizochapishwa zilizoleta dhamila ya kuunda Umoja wa Kikristo, moja ambayo ingefungua mlango wa kukubali Upentekoste. Spurling alihisi kwamba,

1 James Stone, *The Church of God of Prophecy History and Polity* (Cleveland, Tennessee: White Wing Publishing House and Press, 1977), 14.

"Wanamarekebisho walishindwa kuruhusu nafasi ya Uongozi wa Roho Mtakatifu na dhamiri njema."[2] Adrian Varlack, Sr. anabainisha, "Ilikuwa ni hali hii ya mambo, kutokuwepo kwa Roho Mtakatifu, na kukosekana kwa Utiiwa kweli na kuzingatia kwa usahihi Neno la Mungu, hiyo ilichochea mababu zetu wa Kanisa kutafuta ukweli na kujaribu kusimamisha Kanisa la Agano Jipya."[3] Kanisa la mahali hapo lingeanza kuchungwana R.G Spurling; baadaye walianzisha makutano mengine ya Umoja wa Kikristo kulingana na azma yao ya kufuata mwongozo wa Roho.[4]

**Uamsho katika Jumba la shule ya Shearer na Ubatizo wa Moto.**

Mnamo 1896, harakati za kikundi hiki kidogo cha Umoja wa Kikristo kiliguswa na nguvu ya Roho Mtakatifu kwenye uamsho uliofanyika katika Jumba la Shule ya Shearer, katika eneo la Kaunti ya Cherokee, Carolina ya Kaskazini. "Kuonyesha mafundisho na matendo ya harakati za Benjamin Hardin Irwin ya waliobatizwa kwa moto… (uamsho huu) uliipa jamii nguvu na matukio yasiyo ya kawaida."[5] Uamusho huu pamoja na ibada za mara kwa mara ulikuwa na nguvu katika kuhubiri Utakatifu, Utakaso 17 kama baraka ya pili, na Ubatizo na Roho Mtakatifu. Lillie Duggar anabainisha, "Utakaso unaonekanakuwa moja ya mada kuu katika uamsho uliotokea, na watu wengi walitakaswa na damu ya Yesu. Mara tu baada ya Wainjilisti kufunga uamsho, Roho Mtakatifu alidhihirika kwa nguvu katika mikutano ya Maombi iliyokuwa ikifanyika. Watu walipopokea Roho Mtakatifu, walianza kunena kwa lugha zingine."[6] Uamsho katika wa Jumba la Shule ya Shearer, na Kanuni za Kibiblia zilizoingizwa, zilikuwa na athari ya kudumu kwenye harakati za Church of God . Mwanzilishi wa Kanisa la awali, W. F. Bryant, alikuwa akitafuta matokeo ya Utakaso na aliandika, "Wakati huo nilikuwa Mshirika wa Kanisa la Baptist nahakuna hata mmoja wetu aliyeamini Utakaso, japokuwa nilihudhuria uamsho huu. Niliona ni jinsi ganiwale waliokuwa wametakaswa wakienda kwa wenzao na kumaliza tofauti zao zote… Roho ndani yanguilikuwa ikilia, 'nipe baraka kama wale wengine wachache waliopokea.' "[7] Nguvu hii ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu mnamo 1896 ilikuwa utangulizi wa kuingia katika Upentekoste katika mafundisho namatendo.

**Kanisa la Utakatifu katika kambi ya Creek**

Mwanahistoria wa Church of God of Prophecy C. T. Davidson alibainisha:

> Siku ya Alhamisi, Mei 15, 1902, kikundi cha watu kilikutana nyumbani kwa W.F. Bryant, katika Kaunti ya Cherokee, arolina Kaskazini. Richard G. Spurling, Jr

2 Adrian Varlack, *Foundations*, *The Church of God of Prophecy: Concise History, Doctrine, Polity, and Future* (Cleveland, Tennessee: White Wing Publishing House, 2010), 34.
3 Varlack, *Foundations, The Church of God of Prophecy*, 17, 18.
4 Andrea Johnson, Editor, *Servants of the Spirit: Portraits of Pentecostal/Charismatic Pioneers* (Des Moines, Iowa: OBC Publishing, 2010), 41.
5 Vinson Synan, *The Century of the Holy Spirit: 100 Years of Pentecostal and Charismatic Renewal*, 1901-2001 (Thomas Nelson Publishers, 2001), 115.
6 Lillie Dugger, *A. J. Tomlinson: Former General Overseer of the Church of God* (Cleveland, Tennessee: White Wing Publishing House, 1964), 32.
7 Johnson, *Servants of the Spirit*, 41.

alikuwa katikati yao, na akawasimika kama Kanisa la Utakatifu huko kambi ya Creek. Inaonekana kuwa Jumuiya hii ya Kikristo iliwahi kutegemeza Jumuiya nyingine ya Kikristo miaka kumi na sita kabla, lakini katika eneo tofauti. Richard G. Spurling alichaguliwa kuwa Mchungaji, na W. F. Bryant, mmoja wa Maofisa, aliwekwa wazi na Kanisa jipya lililosimikwa, na kuwekwa wakfu, na kuwa taasisi ya kudumu.[8]

Vinson Synan anasema, "Kanisa hili lisingeweza kuwepo kama isingekuwa ziara mnamo mwaka 1903 ya muuzaji wa Biblia anayesafiri kutoka Indiana kwa jina la Ambrose Jessup Tomlinson."[9]

**A. J. Tomlinson na Church of God of Prophecy**

A. J. Tomlinson, mtu asiyekuwa na dhehebu kutoka Indiana, alikuwa mhubiri ambaye alijiunga katika Kanisa la Utakatifu huko Camp Creek.10 Alialikwa kwenye wakati maalum wa kujifunza Neno la Mungu pamoja nyumbani kwa W.F. Bryant mnamo Juni 13, 1903. Tomlinson alilipenda kundi hili, akiwa amewahubiria mara kadhaa, na "alithamini kukaribishwa kwa uchangamfu na upendo waliompa kila wakati (alisema). Walikuwa ni kundi makini na lilitii sana msukumo na maagizo ya Maandiko Matakatifu." Usiku wa Ijumaa ya Juni 12, 1903, Tomlinson aliamua kupanda mlima Burger, nyuma ya nyumba ya Bryant, ili awe na wakati wa kumtafuta Mungu. Huko alikaa usiku katika maombi na, alipokea kile yeye alichokiita maono ya "Kanisa la Mungu la Siku za Mwisho." Tomlinson alishuka chini kutoka mlimani na kuamua kujiunga ushirika na Kanisa la Holiness siku inayofuata ya Juni 13, 1903. Akikumbuka siku hiyo, Tomlinson baadaye alisema:

> Ikiwa utachukua Biblia nzima, ilivyogawanywa sawasawa, hiyo ndio maana halisi ya Church of God. Kwa nini mnataka kuilita Kanisa la holiness la kambi ya Creek? . . . "mmekubaliana kuwahiki nilichosema ndio Kanisa la Mungu, je! mko tayari kukichukua na kuliita Kanisa la Church of God?" Walisema wao walikuwa tayari. Kisha akauliza ikiwa wako tayari kulichukua na kuelewa kwamba HILI NDILO Kanisa la Church of God — si kwamba litakuwa, lakini limeshakuwa Kanisa la Church of God. Walikuwa tayari. Kwa hiyo, nilisimama pale mbele ya mahali pa jiko la moto na Ndugu Spurling, ambaye ameshaenda Mbinguni, alichukua Biblia na kunipa. Alinikabidhi na kusema, "Je! Utachukua hii kama Neno la Mungu, ukiamini na kutenda, kutii maagizo yake na kutembea katika nuru kama Mungu alivyo nuru "Niliwaza kwa kina. Nilikumbuka wakati nilipokuwa juu ya mlima. Nilimaanisha shughuli. Mungu alimaanisha Shughuli.

8 C. T. Davidson, *Upon This Rock, Volume 1* (Cleveland, Tennessee: White Wing Publishing House and Press, 1973), 300.
9 Synan, *Century of the Holy Spirit*, 115.
10 Stone, *The Church of God of Prophecy: History and Polity*, 22.
11 Davidson, *Upon this Rock Volume* 1, 312.
12 Ibid., 312–314.

> Hapa nilitoa mkono wangu kwa Ndugu Spurling… nilichukua jukumu hilo kwa dhati na kwa utakatifu na kuwekwa wakfu, siwezi kusahau kamwe.[13]

